

22C-Maddutw-Twabiy'iy - Maddusw-Swillatis-Sughraa:

i. مَدُّ الصَّلَةِ الصُّغْرَى Maddusw-Swillatis-Sughraa:

Swillah ni kuunganisha herufi ya ه (haa) ya kiwakilishi¹ na herufi ya madd yenye kunasibiyana na *i'raab* yake (dhwammah au kasrah) kitakapokuwa hicho kiwakilishi cha ه ni chenye *i'raab* na kipo baina ya herufi mbili zenye *i'raab*. Swillah hii imegawanyika sehemu mbili mojawapo ni hii ya as-sughraa (ndogo) na ya pili yake ni ya al-kubraa (kubwa) itakayokuja maelezo yake katika Maddul-Far-'iy.

Mfano ya مَدُّ الصَّلَةِ الصُّغْرَى (Maddusw-swillatis-sughraa):

Tarjuma	Kutamkwa kwake	Mfano
Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa	مَا هُوَ ...maalahuw...	الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ ² يَتَرَكِي
... Basi insani pale Mola wake Anapomtia mtihanini, Akamkirimisha (yeye) na Akamneemesha (yeye)...	...رَبُّهُ فَأَكْرَمَهُو وَنَعَّمَهُو... ...Rabbu huw fa-akrama huw wa na'-'ama huw ...	فَأَمَّا آلِنَسْنُنُ إِذَا مَا أَبْتَلَنَهُ رَبُّهُ فَأَكْرَمَهُو وَنَعَّمَهُو ³
Hakika Yeye kwa waja Wake ni ...	إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ Inna huw kaana bi'ibaadi hiy ...	إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَيْرًا بَصِيرًا ⁴

¹ ه (Haa) ya kiwakilishi ni nomino ya mwanamume ya mtu wa tatu (al-ghaaib) katika umoja (فرد) ambayo huwepo mwisho wa neno, yenye kuleta maana 'yeye' au 'yake'.

² Al-Layl (92: 18)

³ Al-Fajr (89: 15)

⁴ Al-Israa (17: 30, 96)

Sharti zake:

- i) Kuweko na *i'raab* (sio sukuwn au herufi ya madd) kabla ya ۞ (haa)
- ii) Kuweko na *i'raab* ifuatie katika neno la pili.
- iii) Haifuatwi na hamzah.

Zinapotimia sharti hizo, basi *i'raab* hizo hutamkwa kwa و (uw) au ي (iy) na kuvutwa kwake ni harakah mbili.

Istithnaa (Maneno yenye kwenda nje ya hukmu hii):

Maneno mawili pekee katika Qur-aan ambayo huwa hayafuati hukmu hii, kwa sababu ndivyo ilivyopokelewa kutoka riwaayah ya Hafsw 'an 'Aaswim *twariyq-Shaatwibiyyah*. Mojawapo ni kuvutwa kama inavyovutwa **مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى** (maddusw-swillatis-sughraa) japokuwa halina swiffah wala sharti za **مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى** (maddusw-swillatis-sughraa). La pili yake bila ya kuvutwa mvuto wa **مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى** (maddusw-swillatis-sughraa) huku likiwa na swiffah za sharti za **مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى** (maddusw-swillatis-sughraa). Nayo ni yafuatayo:

Hukmu haitimizwi		Hukmu inatimizwa	
<p>يَرْضَاهُمْ ... yardhwahu lakum Bonyeza usikilize</p>	<p>وَإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ⁵</p>	<p>فِيهِ ... fiyhiy muhaanah Bonyeza usikilize</p>	<p>وَتَحَلَّدَ فِيهِ مَهَانًا⁶</p>
<p>Haivutwi ۞ juu ya kuwa iko baina ya herufi mbili zenye <i>i'raab</i>.</p>		<p>Huvutwa ۞ juu ya kuwa herufi iliyoko kabla yake ni sukuwn.</p>	

⁵ Az-Zumar (39 : 7)

⁶ Al-Furqaan (25: 69)

--	--